# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

### Kikao cha Kwanza – Tarehe 28 Januari, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ZILIIMBWA

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina taarifa hapa ama ninazo taarifa ambazo ninataka kuwapa kwa asubuhi hii; lakini taarifa ya kwanza, Waheshimiwa Wabunge mara baada ya kuahirisha Mkutano wetu wa Kumi na Saba, tulipata jambo la kuhuzunisha kwa Bunge na Taifa kwa ujumla. Usiku wa kuamkia tarehe 27 Novemba, 2024 tulipata msiba mkubwa wa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)*, Kanda ya Afrika, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile.

Hayati Mheshimiwa Dkt. Ndugulile alifia Nchini India alipokuwa akipatiwa matibabu. Aliagwa rasmi tarehe 2 Disemba,

2024 katika Viwanja vya Karimjee, Jijini Dar es Salaam katika shughuli iliyoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na mazishi ya mpendwa wetu yalifanyika tarehe 3 Disemba, 2024. Mazishi haya yalifanyika katika makaburi ya Mwongozo, Wilaya ya Kigamboni, Jijini Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa aliongoza mazishi haya na pia nilihudhuria pamoja na Wabunge ambao walipata fursa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo desturi yetu na kwa heshima ya Mbunge mwenzetu ambaye tumempoteza, Hayati Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, ninaomba tusimame kwa dakika moja ili kumkumbuka na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, apokelewe.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kama ishara ya kumkumbuka na kumwombea Hayati Dkt. Faustine E. Ndugulile)*

**SPIKA:** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Waheshimiwa Wabunge, nina taarifa nyingine, ninapenda kutumia fursa hii kuwataarifu kuwa Ofisi ya Bunge imepata tuzo ya Mshindi wa Kwanza wa Taarifa Bora ya Hesabu za mwaka 2023. Hii nafasi ya kwanza ni kwa kundi la Wizara na Idara nyingine za Serikali. Tuzo yenyewe inaitwa *The First Winner for the Best Presented Financial Statement Awards for the Year 2023 in the Ministries and Other Government Department Category*. Tuzo hii imetolewa tarehe 29 Novemba, 2024 na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi *(The National Board of Accountancy and Auditors (NBAA))*. Tuzo hii ilitolewa wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wahasibu na Wakaguzi uliofanyika Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuzo hii ya utayarishaji bora wa hesabu ambayo ofisi yetu imepata, hutolewa kila mwaka na *NBAA* kwa lengo la kuhamasisha Wizara, Idara, Taasisi, Mikoa, Mashirika na Kampuni Binafsi kuzingatia viwango wa kimataifa

katika uandaaji wa hesabu. Kwa maana hiyo, Mhimili wa Bunge umeonesha mfano bora wa kusimamia weledi wa Wahasibu na Wakaguzi katika kusimamia mali za umma kwa kuzingatia pia Bunge linajukumu la kusimamia taasisi nyingine za umma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza sana Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, lakini pia Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Bunge, *CPA* Layson Mwanjisi na watumishi wote wa Bunge kwa kazi nzuri iliyofanyika ya uandaaji bora wa hesabu uliosaidia kupata tuzo hii. *(Makofi)*

Nitoe rai kwa Wahasibu na Wakaguzi wote nchini, kuendelea kufanya kazi zao kwa ufanisi kila mwaka wa fedha ili kuondoa changamoto za matumizi mabaya ya fedha za umma.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimalizie kwa kuwaonesha tuzo ambayo iko hapa mezani. Sasa haya maneno nilikuwa nimeshawasomea awali, ngoja nisome kwa Kiswahili halafu ndio niwaoneshe. Japokuwa niliwashawasomea kwa Kiingereza, sasa kwa Kiswahili inaitwa Tuzo ya Mshindi wa Kwanza wa Taarifa Bora ya Hesabu za mwaka 2023. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii ndiyo tuzo yetu tuliyoipata kwa nafasi ya kwanza na ninafikiri pongezi nilizompa Katibu zimeendana na hayo makofi ambayo mmeyatoa. Kwa kweli tumpongeze sana Katibu wetu wa Bunge kwa usimamizi mzuri wa zoezi hili zima. Pia niwapongeze na ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa maana kuna majukumu mbalimbali huwa mnapewa huko kwenye Kamati, maana yake yale mnayotakiwa kuyafanya basi mnayafanya vizuri ndiyo maana ofisi yetu imefika sehemu hii. Kwa hiyo, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Pia ninawashukuru na ninyi kwa sababu yako mambo mengi ambayo kama tungekuwa hatufuati utaratibu wa kumdai Mhasibu wetu Mkuu wa Bunge ingeleta mushkeli kidogo huku. Kwa hiyo, nanyi niwapongeze kwamba mnadai madai mnayostahili, kwa hivyo tumepata tuzo hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 1

**Fedha za Kukamilisha Kituo cha Afya Kisiwani – Same Magharibi**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha katika Kituo cha Afya Kisiwani – Same ili kukamilisha ujenzi wa majengo muhimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na 2021/2022 Kituo cha Afya Kisiwani kilipokea jumla ya shilingi milioni 490 kwa ajili ya ujenzi wa majengo matano ambayo ni: Jengo la Maabara; Jengo la kufulia; Jengo la Upasuaji; Jengo la Wazazi; Kichomea taka; na nyumba ya mtumishi *(three in one (3 in 1))*. Majengo yote yamekamilika na yanatoa huduma ikiwemo huduma za dharura na upasuaji kwa mama mjamzito.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya ujenzi wa kituo hiki itahusisha ujenzi wa wodi ya wanawake, wanaume na watoto.

Serikali itaendelea kutekeleza ujenzi huu kwa awamu na Kituo cha Afya cha Kisiwani kitapewa kipaumbele. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa kituo hiki kinahudumia kata tatu: Kata ya Mshewa, Msindo na Kisiwani hivyo kina wananchi wengi sana ambao wanahudumiwa katika kituo hiki; na wodi ya wanawake na wanaume hazipo kabisa hivyo, anapotokea mgonjwa ni lazima apelekwe katika Hospitali ya Wilaya ya Same, kilometa 30. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha ujenzi wa majengo haya ili kusogeza huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kituo hiki kiko karibu na makaburi, kwa sababu hiyo wagonjwa waliolazwa pale hususan wodi ya mama na mtoto wanaona matukio yote ambayo yanaendelea wakati wa mazishi, hivyo huwa na hofu sana. Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga uzio kwa haraka katika kituo hiki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana na uhitaji wa kituo hiki cha afya na ndiyo maana tayari Serikali ilishaleta shilingi milioni 490 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya awali. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea na awamu ya pili, ambapo Serikali italeta fedha kwa ajili ya kujenga wodi ya wanawake, wanaume pamoja na watoto.

Serikali itafanya hivyo kwa kuzingatia umuhimu mkubwa sana wa huduma inayotolewa katika kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili ambalo linahusiana na suala zima la uzio. Ninaomba nichukue nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wajibu wa msingi, aweze kufanya tathmini katika eneo la hiki kituo cha afya ili ajue gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa *fence* na kupitia mpango na bajeti katika halmashauri inayotokana na mapato ya ndani, waweze kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga uzio huu na pale nguvu itakapopungua Serikali Kuu itakuja kuongezea lakini, Mkurugenzi aanze kazi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona leo sitaki historia, sitaki kujenga hoja, nenda moja kwa moja kwenye swali. Ukianza tu kujenga hoja ninazima *mic*, ninampa anayefuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ninaomba kuuliza swali la nyongeza, Tarafa ya Mgeta ina kata saba na ina kituo kimoja cha afya....

**SPIKA:** Swali.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza swali, je, ni lini Serikali itatuongezea Kituo kingine cha Afya katika Tarafa ya Mgeta?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya uwakilishi anayoifanya katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie kwamba, katika mwaka huu wa fedha Serikali italeta fedha za kuanzia, shilingi

milioni 250 kwa ajili ya kuanza kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika kila jimbo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, ninaomba nikuhakikishie na wewe utakuwa miongoni mwa Wabunge watakaopokea fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye majimbo yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kujenga Kituo cha Masieda – Gembakw, ambako tulishaweka kwenye mpango wa kujengewa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wabunge wote wamepokea pongezi zako za maswali na nimeshapokea shukurani zenu za nafasi ninazowapa. Mheshimiwa Naibu Waziri, moja kwa moja kwenye majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyotangulia kusema, kwamba katika mwaka huu wa fedha Serikali italeta shilingi milioni 250 za kuanza ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati katika kila jimbo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na yeye katika jimbo lake fedha hizi zitamfikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italeta fedha za kujenga kituo cha afya katika Tarafa ya Nambis, ambako ni miaka minne tumeomba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Zacharia Issaay kwamba katika mwaka huu wa fedha shilingi milioni 250 zitapelekwa katika jimbo lake kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka pesa katika Kata ya Image? Kwa sababu wodi na maabara zinatakiwa ili wananchi wasiende umbali mrefu kufuata matibabu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuendelea kuimarisha miundombinu katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari fedha zimekuwa zikitoka kwa awamu kwa ajili ya kuboresha vituo vyetu hivi vya kutolea huduma za afya msingi. Nimhakikishie Serikali itaendelea kuleta fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu aliyoitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya kumalizia jengo la *OPD* katika Kituo cha Afya cha Chiungutwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mchungahela kwamba, Serikali tayari imekuwa ikileta fedha, kwa ajili ya kuanza kujenga majengo ya awali. Pia Serikali inajenga miundombinu hii katika vituo vyetu hivi vya afya na vituo vya kutolea afya msingi kwa awamu. Nimhakikishie, kwa awamu inayofuata Serikali itaweka kipaumbele kikubwa sana, kwa ajili ya kukamilisha majengo haya ya *OPD* katika kituo hiki cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali italeta fedha kwenye Kituo cha Afya Nyang'hwale, kwa ajili ya kujenga jengo la *X–Ray?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Hussein Amar kwamba, Serikali inaleta fedha kwa awamu, kwa ajili ya kuendeleza miundombinu katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi. Pia, kama alivyoainisha, Jengo hili la *X–Ray,* Serikali italeta fedha, kwa ajili ya kuhakikisha linajengwa, ili liweze kuanza kutoa huduma hizi kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kujenga majengo muhimu katika Kituo cha Afya cha *Mile* Tano, Jimbo la Tabora Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kwamba, Serikali inajenga miundombinu katika vituo vyetu vya kutolea afya msingi kwa awamu. Tayari imejenga majengo ya awali na inaendelea kuleta fedha kwa awamu, kwa ajili ya kuboresha na kukamilisha miundombinu mingine katika vituo vyetu hivi vya kutolea huduma ya afya msingi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge fedha zitapelekwa kwa ajili ya kuendeleza kujenga miundombinu katika kituo hiki cha afya alichokitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali italeta fedha, kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa jengo la *theatre* katika Kituo cha Afya Ntuntu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mtaturu kwamba, Serikali inafahamu umuhimu mkubwa sana wa vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi na ndiyo maana inaleta fedha kwa awamu, kwa ajili ya kuvijenga na kuviendeleza vituo hivi. Kwenye hicho kituo cha afya alichokitaja na jengo hili la *theatre,* nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itapeleka fedha, kwa ajili ya kuhakikisha jengo hili linajengwa ili kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ezra Chiwelesa.

**MHE. *ENG*. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, Vituo vya Afya vya Kalenge na Nyabusozi, vilitengewa pesa kiasi cha shilingi milioni 500. Je, ni lini pesa hii italetwa, kwa ajili ya ukarabati wa vituo hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Ezra Chiwelesa kwamba, Serikali ina nia thabiti ya kuhakikisha inaimarisha utoaji wa huduma za afya msingi na ndiyo maana inaleta fedha, kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika vituo hivi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali itaendelea kuleta fedha kwa awamu kama ilivyotanguliza kuleta fedha za awali kwa awamu iliyopita. Pia, awamu inayofuata fedha zitakuja, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, vituo hivi vinaendelea kuboreshwa na vinajengwa ili wananchi waweze kupata huduma bora.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. *ENG*. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hii nauliza mara ya tano, *seriously*. Kata ya Kihagara watu wanalala watano, wanne, kwenye kitanda. Ni lini wodi itajengwa katika Kijiji cha Kihagara, kwa ajili ya Kituo cha Afya Kihagara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya, kama unauliza mara ya tano ni swali la nyongeza, nafikiri lije la msingi ili ujibiwe swali lako kikamilifu, kwa sababu, kama ni mara ya tano, halafu unauliza kitu hicho hicho na bado majibu hayajakutosheleza, nashauri swali lako lije kama swali la msingi uweze kupata majibu mahususi, kwa ajili ya hicho kituo cha afya.

**MHE. *ENG*. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ni pamoja na maswali ya msingi.

**SPIKA:** Ulishauliza, hayo ni ya msingi?

**MHE. *ENG*. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nasema nilishauliza pia, swali la msingi kuhusiana na suala hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie pia, Mheshimiwa *Engineer* Manyanya kwamba, nia ya Serikali ni kuhakikisha inaendelea kuboresha huduma za afya msingi. Ndiyo maana Serikali inatoa fedha kwa awamu, kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika vituo vyetu vya afya, hospitali na zahanati.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kupitia Serikali Kuu na kupitia mapato ya halmashauri itaendelea kuleta fedha kwa awamu, kwa ajili ya kuendelea kuimarisha na kukamilisha miundombinu yote inayohitajika, ili wananchi waweze kupata huduma iliyo bora katika kituo hiki alichokitaja, Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama ni uhalisia Mheshimiwa Mbunge ameuliza na hii ni mara ya tano, ni dhahiri iko sababu ya kupata majibu mahususi kwamba, ni lini hiyo wodi; Mheshimiwa Stella, umesema ni wodi?

Kuna haja ya kupata majibu mahususi kuhusu hiyo wodi. Kama ni halmashauri inajenga au ni Serikali Kuu ama ni nani anajenga, nafikiri kuna umuhimu huo. Kwa sababu, kuuliza swali la kitu hichohicho mara tano, kidogo inakuwa inaleta changamoto.

Swali la mwisho la nyongeza kwenye hili, Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Ni lini Serikali itajenga majengo ya watumishi na *mortuary* katika Kituo cha Afya cha Uru Kusini ili kiweze kuleta tija?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Felista Njau kwamba, Serikali inaendelea kuhakikisha inaimarisha huduma za afya msingi kwa kuendelea kujenga miundombinu imara, mizuri na kuikamilisha yote, ili wananchi waweze kupata huduma bora. Ninaomba nimhakikishie, Serikali itatenga fedha kila mwaka wa bajeti kupitia Serikali Kuu na kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri, kwa ajili ya kuhakikisha inakuja kujenga na kukamilisha majengo aliyoyataja, Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Kuboresha Miundombinu ya Shule za Tarafa ya Ngorongoro**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kupeleka huduma za jamii na kuboresha miundombinu ya shule zilizobaki katika Tarafa ya Ngorongoro?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kupeleka huduma za jamii na kuboresha miundombinu ya shule katika maeneo yote yenye uhitaji, ikiwemo Tarafa ya Ngorongoro ambapo mwaka 2021/2022 hadi mwaka 2023/2024 Serikali imetumia jumla ya shilingi bilioni 7.9 za ruzuku ya elimu bila malipo katika Tarafa ya Ngorongoro. Aidha, mwaka 2024/2025, Serikali imetoa shilingi bilioni 1.7 za ruzuku ya elimu bila malipo, kwa ajili ya kuboresha huduma za elimu katika Tarafa hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile halmashauri kupitia mapato ya ndani, mwaka 2024/2025 imetoa jumla ya shilingi milioni 120, kwa ajili ya kukarabati miundombinu katika katika Shule za Msingi Alailelai, Sendui, Olchanimerock, Naiyobi, Nainokanoka, Olbalbal, Ngoile, Moklal na Oloilob.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na jitihada hizi za Serikali, bado mazingira ya shule alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ni mabovu. Ninaomba, ikimpendeza, aweze kuzitembelea na kujionea mazingira halisi.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; je, ni lini ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ngorongoro utafanyika na Serikali ikiwemo kuongeza mabweni?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Shule ya Sekondari ya *Rift Valley,* Wilayani Monduli, wana changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama. Je, ni lini Serikali itawachimbia kisima hawa wanafunzi wetu ili waweze kusoma vizuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na kufika, ili kujionea hali halisi katika Tarafa hii ya Ngorongoro, kwa maana ya Sekta hii ya Elimu. Pia, kuhusiana na swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge, ninaomba nimhakikishie kwamba, Serikali inaendelea kutenga fedha. Kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba, kupitia mapato ya ndani tayari kuna milioni 120 ambazo zimetengwa katika mwaka huu wa bajeti, ili kuhakikisha zinakarabati miundombinu katika shule.

Mheshimiwa Spika, Desemba, 2024, kupitia fedha shilingi milioni nane, matundu nane ya vyoo yamejengwa katika shule hiyo. Pia, tuna shilingi milioni 100 ambazo zipo, kwa ajili ya ujenzi wa bwalo. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuendelea kumsisitiza mkurugenzi na timu yake ya elimu, waweze kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu hii, ili iweze kukamilika kwa wakati na wanafunzi wetu waweze kupata mazingira bora ya kusomea.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Zaytun Swai, kuhusiana na Shule hii ya *Rift Valley* ambayo haina kisima na haina maji; tayari Serikali imeshasambaza mitambo ya kuchimba visima, kila mkoa umepata mitambo hii, kwa ajili ya kuchimba visima. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumkumbusha mkurugenzi wajibu wa msingi, yeye pamoja na timu yake, waweze kufanya mawasiliano na Mamlaka ya Maji ya Mkoa, kupitia Ofisi ya *RAS*, ili waweze kuchimba kisima kwa gharama nafuu, ili wanafunzi wetu katika Shule hii ya *Rift Valley* waweze kupata maji na wawe na mazingira ya kusomea na walimu wawe na mazingira mazuri ya kufundishia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, ni lini miundombinu ya Shule ya Msingi Iyendwe, Siliwiti, Sanja, Mfuto pamoja na Ipatikana itaboreshwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia miradi mbalimbali, ukiwemo Mradi wa *SEQUIP* wa gharama ya jumla ya shilingi trilioni 1.2 na kupitia mapato ya ndani, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu katika Sekta ya Elimu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari tumekuwa tukileta fedha kila awamu, kila mwaka wa bajeti, kwa ajili ya kuendeleza miundombinu katika Sekta ya Elimu. Nimhakikishie, Serikali itaendelea kufanya hivyo, ili kuzifikia shule hizi alizozitaja, ili ziweze kupatiwa miundombinu bora na wanafunzi wetu wapate sehemu nzuri ya kujifunzia na walimu wapate sehemu nzuri ya kufundishia.

**SPIKA:** Mhe. Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Shule ya Sekondari *SUA* maboresho yake yatakamilika, hasa ujenzi wa maabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Chiristine Ishengoma kwamba, Serikali inaendelea kuleta fedha kwa awamu, kwa ajili ya kukamilisha miundombinu katika Sekta ya Elimu. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali italeta fedha, kwa ajili ya kukamilisha miundombinu hii ya maabara, ili wanafunzi waweze kupata miundombinu bora ya kupatia elimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye shule kongwe zilizopo katika Jimbo la Newala Vijijini, ili ziweze kuboreshwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba, kuna shule ambazo ni kongwe, miundombinu yake imechakaa na inahitaji ukarabati au ujenzi wa shule mpya. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Maimuna Mtanda kwamba, Serikali kila mwaka wa fedha inafanya ukarabati katika shule zetu Kongwe.

Mheshimiwa Spika, nitakaa na Mheshimiwa Mbunge tutaongea kwa karibu, ili aweze kunieleza vipaumbele katika jimbo lake, ili katika mgao naye aweze kupata ujenzi na ukarabati wa shule hizi kongwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Omuchwekano na Shule ya Msingi Kitwechenkura zimechakaa majengo, lakini pia, vyoo vikiwa vimekaribia kujaa. Ninataka kujua mkakati wa Serikali wa kuboresha majengo na pia, huduma ya vyoo ambavyo kwa sasa vinafurika na hakuna maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nia na madhumuni ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, inaboresha miundombinu katika Sekta ya Elimu kwa kuboresha ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama vile madarasa, kujenga mabweni, kukarabati vyoo na kadhalika. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili ni jukumu la msingi kabisa la Serikali na Serikali itaendelea na wajibu huo na kuja kuzifikia shule hizi ulizozitaja ambazo zina mazingira ambayo

siyo mazuri kwa wanafunzi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali itafika kwenye shule hizo na itapeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha zinakarabatiwa.

Na. 3

**Ujenzi wa Daraja Katika Mto Ruvuma**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga fedha za kujenga Daraja la Kijiji cha Lihale na Lusonga katika Mto Ruvuma, ili kuunganisha Mbinga Vijijini na Peramiho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na kazi za upembuzi yakinifu katika Daraja la Lusonga katika Mto Ruvuma, ili kujenga daraja kubwa la kudumu. Aidha, katika mpango na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali imeweka katika mipango yake ujenzi wa daraja la waenda kwa miguu *(suspension foot bridge)* na pikipiki kwa gharama ya shilingi milioni 175.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri yenye kutia moyo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, daraja hili kila mwaka limekuwa linapoteza watu na hivi karibuni watu watatu wamekufa maji watatu. Je, Serikali kupitia Jeshi la Wananchi haiwezi kutuletea daraja la dharura ili liweze kupitika wakati huu tukisubiri mipango mizuri ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali ilitenga fedha shilingi bilioni mbili, kwa ajili ya kujenga daraja la kuunganisha Kingoli, Kata ya Litumbandyosi pamoja na Kijiji cha Machimabharafu,

Ibumi, Wilaya ya Ludewa, kwa muda mrefu ujenzi wa daraja hili unasuasua. Je, lini sasa daraja hili litakamilika ili kuleta furaha kwa wananchi hawa, wafa maji karibu kila mwaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza alilosema kuhusu jeshi, nadhani ni lazima kufanya mawasiliano, kwa hiyo, jibu swali la pili. Hilo la kwanza atakupa majibu akishawasiliana na watu wa jeshi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali la pili la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, napokea masikitiko yake kuhusu changamoto wanazopitia wananchi wake katika Jimbo hili la Mbinga Vijijini. Ninaomba nimpe faraja Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tayari imeshatenga bajeti ya shilingi bilioni 2.9, kwa ajili ya kujenga Daraja katika Mto Ruhuhu. Mpaka muda huu tayari shilingi bilioni 1.9 zimeshatengwa na tayari awamu ya kwanza ya ujenzi inatarajiwa kukamilika mwezi wa nane mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nichukue nafasi hii kumkumbusha Meneja wa *TARURA* wa Mkoa na wa Wilaya, waweze kusimamia utekelezaji wa mradi huu ili uweze kwisha kwa wakati na wananchi waweze kutumia Daraja hili la Mto Ruhuhu waepukane na changamoto na adha wanazozipata kutokana na mazingira yaliyopo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Timu ya Wilaya na ya Mkoa ya *TARURA* imepokea maelekezo haya kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa mradi huu kwa haraka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italeta fedha, kwa ajili ya ujenzi wa madaraja zaidi ya 10 yaliyoathiriwa na Mvua za *El-Nino* katika Barabara ya Ntikimwaga – Tandawale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa fedha kwa utaratibu wa fedha za dharura. Mpaka sasa hivi Serikali imetumia jumla ya shilingi bilioni 84, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ambayo imeharibiwa na mvua za *El-Nino*. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inaendelea kufanya mapitio na tathmini, ili iweze kufikia maeneo mengi zaidi ambayo yameathirika na mvua za *El-Nino*. Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie Serikali itafika katika madaraja aliyoyataja ili iweze kuyafanyia ukarabati na wananchi waweze kupata miundombinu bora.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutoka Kiponzero kwenda Wasa ina mashimo makubwa sana. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za dharura ili tutengeneze makalavati na kufukia hayo mashimo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la msingi linahusu madaraja. Sasa hayo mambo ya mashimo, barabara sijui imefanyaje, mnamweka Naibu Waziri katika mazingira magumu, amejiandaa kujibu swali linalohusu madaraja. Hata hivyo, kwa sababu nilikuwa sijatoa ufafanuzi; swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kalenga, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwake.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Kiswaga kwamba, Serikali itaendelea kufikia maeneo mbalimbali ambayo yameathirika, pamoja na barabara ambazo zimeathirika kwa kiwango kikubwa, ili kuweza kuzirekebisha na kuweza kupitika. Kila mwaka wa bajeti, Serikali inatenga shilingi bilioni 21, kwa ajili ya fedha za dharura, ili kufikia maeneo kama haya. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itakuja kufika katika Jimbo lako kwenye maeneo uliyoyataja, kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya barabara hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italijenga upya na kwa ubora zaidi, Daraja la Mto Maloha ambalo hivi karibuni lilisombwa na mafuriko na kusababisha kukatika kwa mawasiliano katika Kata za Bugando na Mwabanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mazingira ambayo yanajitokeza, ambapo madaraja yanasombwa na maji, miundombinu inaharibika na mawasiliano yanakatika. Serikali inachukua hatua za dharura na mpaka sasa Serikali imeshatumia jumla ya shilingi bilioni 84 kwa ajili ya kuhakikisha inarudisha mawasiliano maeneo ambayo yameathirika, madaraja yamekatika na hamna mawasiliano. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge dhamira hiyo ya Serikali itaendelea na itakuja kufika katika Jimbo lako kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu ya daraja alilolitaja inarejeshwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Abdul – Hafar Idrissa Juma, Mbunge wa Mtoni, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Kukarabari Taa za Barabarani**

**MHE. ABDUL – HAFAR IDRISSA JUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa taa za barabarani zilizoharibika kwa kugongwa au hitilafu nyingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kushughulikia masuala ya usalama barabarani ikiwemo kuweka na kukarabati taa za barabarani zilizoharibika kote nchini. Kwa sasa, *TANROADS* ipo katika hatua ya manunuzi ya kuwapata wakandarasi watakaofanya kazi hiyo. Baada ya kukamilika kwa hatua ya manunuzi na wakandarasi kupatikana, kazi ya ukarabati na uwekaji wa taa hizo itafanyika kulingana na mahitaji ya kila Mkoa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul – Hafar Idrissa Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL – HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha sasa tumeshazidi nusu. Je hiyo hatua ya manunuzi itaisha lini maana kiza kimezidi katika baadhi ya barabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimwa Spika, labda tu nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kulikuwa na changamoto kubwa kwamba taa zilikuwa nyingi zinatofautiana na hazina *standard*. Kwa hiyo, tumeamua kununua kwa pamoja ili taa hizo ziwe katika ubora unaolingana katika nchi yote, ndiyo maana huo mchakato umechukua muda mrefu, lakini nimhakikishie kwamba tunavyoongea huu ni mwezi wa kwanza na tunaweka kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha huu tutakuwa tumerudisha taa zote ambazo zina uharibifu kwa namna yoyote ama zimegongwa ama zimeharibika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimwa Spika, je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kufunga barabara katika Mji wa Mbinga? Ahsante.

**SPIKA:** Kufunga barabara ama kufunga taa?

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimwa Spika, kufunga taa katika Mji wa Mbinga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi tumepata mahitaji ya Mikoa yote na Miji yote ambayo haina taa, ndiyo maana tunanunua taa kwa pamoja nikiamini kwamba Mji wa Mbinga nao utanufaika kupewa taa hizo kama Mji wa Mbinga una mahitaji ya hizo taa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itamalizia kufunga taa katika Mji wa Tinde hasa kutoka njia panda kwenda Kahama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mahitaji ya taa yanaletwa na mkoa na Meneja wa Mkoa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepata orodha ya mahitaji ya taa zote za barabarani, kwa hiyo ina uhakika na Mji wa Tinde utakuwa ni mji mmojawapo ambao utapata hizo na tutakuja kukamilisha kufunga hizo taa ambazo bado. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimwa Spika, nini mpango wa Serikali kukarabati taa zilizoharibika za barabarani katika barabara za *TANROADS* Wilaya ya Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata katika jibu langu la msingi nimesema taa zote ambazo zimeharibika, zimegongwa ama hazifanyi kazi zimeshaainishwa na ndiyo maana tumenunua kwa pamoja ili ziende zikafungwe ikiwepo na Mji wa Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na hayo majibu ninaona Wabunge bado wamesimama. Mheshimiwa Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimwa Spika, ahsante. Ni lini mkandarasi anaeweka taa katika Wilaya ya Nanyumbu atalipwa fedha zake ili kazi iendelee?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimwa Spika, ahsante. Ninaomba tu nilichukue hilo la Mheshimiwa Mbunge nijue changamoto ni nini. Kwa sababu tunachojibu hapa ni taa ambazo zimeharibika ama zimegongwa, kwa hiyo masuala ya malipo nitaomba baada ya hapa niweze kuongea na Mheshimiwa Mbunge ili nimpe jibu sahihi ni kitu gani kimekwamisha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimwa Spika, Mji mdogo wa Iguguno una kipande cha kilomita moja tu ya lami, lakini hauna taa. Je, ni lini angalau mtatufariji tu kwa taa maana yake barabara yote hiyo ni ya vumbi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tumesema mara kadhaa kwamba miji yote mikubwa na miji ambayo inakua itawekewa taa nina hakika hata Mji wa Iguguno ambao unakua utakuwa upo kwenye huo mpango na hasa kama Mheshimiwa Mbunge alifikisha ama Meneja wa Mkoa atakuwa ameleta

maombi, kwa sababu tumekusanya maombi yote ya miji ambayo inakua ili iweze kuwekewa taa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 5

**Ujenzi wa Barabara za Zege Maeneo Korofi**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara kwa kutumia zege sehemu korofi ili kuepuka matengenezo ya mara kwa mara na upotevu wa fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuboresha sehemu korofi katika barabara kama vile milima mikali, Mbuga na sehemu zenye udongo wa mfinyazi. Hatua hizo ni pamoja na ujenzi kwa kutumia zege, ujenzi kwa kutumia mawe na kadhalika. Pamoja na kuzingatia mahitaji, lakini pia uamuzi wa ujenzi wa aina gani utatumika kuzingatia gharama za upatikanaji wa mali ghafi za ujenzi zinazopatikana kwa urahisi katika eneo husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimwa Spika, namshukuru Waziri kwa majibu yake, upatikanaji wa malighafi kama alivyosema, sasa kwa kuwa vifaa vya kujenga barabara kwa zege hupatikana hapa Tanzania, tofauti na lami ambayo huagizwa kutoka nje. Sasa Serikali haioni iko haja kwamba zitaokolewa fedha nyingi na hivyo kuongeza barabara nyingi zaidi kujengwa badala ya kendelea na kutumia lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimwa Spika, ni kweli kwamba zipo malighafi ambazo zinapatikana Tanzania, lakini ninataka tu nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapoongelea zege si vifaa vyote vinapatikana hapa ndani. Vinavyopatikana ndani hapa ni mawe lakini *cement* pamoja na nondo ni vitu ambavyo lazima uvitumie kwenye ujenzi wa barabara ya zege na zege ina gharama kubwa zaidi kuliko aina ya lami, ndiyo maana tuna barabara chache sana tulizojenga kwa zege na gharama yake inaweza ikawa zaidi ya mara mbili na nusu kuliko barabara ya kawaida ya lami ukijenga kwa zege. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri *cement* na nondo si zinapatikana hapa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimwa Spika, zinapatikana hapa lakini gharama yake unapojenga barabara maana yake ni kama unajenga msingi wa nyumba na ndiyo maana tuna barabara kwa mfano ile inayoenda Ludewa wakati huku unaweza ukajenga kilomita moja pengine bilioni moja na nusu kwa kilomita ile inakwenda si chini ya bilioni tatu kwa kilomita moja kwa sababu ya ujenzi wake unavyokuwa. Ahsante.

**SPIKA:** Hiyo sehemu ya gharama imeeleweka, mwanzoni pale wakati ukianza kujibu umesema kuna vitu vinapatikana nchini halafu sasa ndiyo nikawa najiuliza *cement* na nondo havipatikani hapa? Kwa hiyo, umeeleweka kwamba vinapatikana hapa, lakini ni ghali kujengea barabara, hilo limeeleweka.

Mheshimiwa Tumaini Magessa, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kwa lami kutoka Mpomvu kwenda Kakora na kutoka Katoro kwenda Ushirombo? Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimwa Spika, ninaomba nimwombe Mheshimiwa Magessa Mbunge wa Busanda. Kwenye majibu yangu yalikuwa yanazungumzia maeneo korofi ambayo yanahitaji ujenzi wa zege. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge ili nimjibu vizuri kwa uhakika labda baada ya hapa niweze kujua hiyo barabara ambayo anaiongelea kwa ujenzi wa kipande cha lami, tuongee naye nijue tuko hatua gani kwa sababu tayari ipo kwenye mpango wa ujenzi nijue tuko kwenye hatua gani ili niweze kumpa jibu linaloeleweka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mansoor, swali la nyongeza.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunayo Barabara ya kutoka Hungumalwa, Ngudu kuelekea Magu kilomita 71, Mkandarasi yuko amepewa mkataba wa kujenga barabara ya kilomita 10, ana mwaka mzima anasubiri fedha ili aanze kujenga barabara. Ninaomba kujua Serikali itatoa fedha lini mkandarasi aanze kujenga barabara? Ahsante.

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Mbunge hilo lije kama swali la msingi kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amejiandaa kujibu maswali yanayohusu barabara ya zege sehemu korofi. Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa kwenye Barabara kuu ya Chalinze, Segera, Korogwe, Mombo, Same na Himo?

**SPIKA:** Maeneo korofi Mheshimiwa?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii inahitaji ukarabati mkubwa maeneo mengi ni korofi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwanza hiyo barabara aliyoitaja ni barabara ya zamani ambayo pia ni

barabara ambayo ni nyembamba sana. Sasa hivi tumeshafanya usanifu wa barabara yote ambayo itakuwa ni kuifanyia ukarabati mkubwa kama kuijenga upya kwa sababu ya hali yake na vile ambavyo ni nyembamba inatakiwa ukarabati mkubwa wala siyo kujenga eneo korofi ni kama barabara yote inatakiwa ikarabatiwe. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake.

Na. 6

**Kudhibiti Wizi wa Mifugo Rorya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini wizi wa mifugo utadhibitiwa Wilayani Rorya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lina wajibu wa kudhibiti wizi wa mifugo katika Wilaya ya Rorya. Jitihada zinazofanywa na Jeshi la Polisi ni pamoja na kutoa elimu juu ya ulinzi jirani, kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi na mazizi salama. kuimarisha kikosi cha kupambana na wizi wa mifugo kwa kuongeza askari na vitendea kazi, kufanya mikutano ya ujirani mwema na Polisi Wilaya ya Nyatike ya Nchini Kenya juu ya udhibiti wa makosa yanayovuka mipaka na jitihada zote hizi ni endelevu na zimepunguza kwa kiasi kikubwa wizi wa mifugo. Aidha, takwimu zinaonesha katika kipindi cha mwezi Disemba, 2023 na mwezi Januari, 2024 kumeripotiwa matukio 26 na kipindi kama hicho mwezi Disemba, 2024 na mwezi Januari, 2025 kumeripotiwa matukio tisa, sawa na upungufu wa matukio 17. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na jitihada hizi zinazofanywa na Jeshi la Polisi kudhibiti wizi wa mifugo, lakini bado wizi huu upo na unaathiri kwa kiasi kikubwa sana wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ninataka nijue kama Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuja na njia mbadala badala ya hizi zilizozoeleka ili kuweza kudhibiti wizi wa mifugo kwa sababu imechukua zaidi ya miaka 20 sasa kwenye eneo eneo lile?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa changamoto kubwa ni pamoja na ukosefu wa vitendeakazi hasa magari ya doria. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kupeleka magari hasa kwa vituo vyote vitatu kwa maana ya Kinesi, Utegi na Shirati ili kuendelea kudhibiti wizi wa mifugo kwenye eneo lile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwa sasa njia ambayo tungependekeza ni kuimarisha ulinzi shirikishi pia kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wetu kuhusu suala zima la wizi wa mifugo katika eneo hili la Rorya.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili kuhusu vitendeakazi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Jeshi la Polisi limeagiza magari ya kutosha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaimarisha ulinzi na usalama maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Rorya. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ninataka kujua ni vipi Serikali imejipanga kudhibiti wizi wa binadamu kwa jina maarufu la utekaji katika nchi yetu, hasa ukizingatia sisi Iringa Mjini ni wahanga? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu, hebu rudia swali lako.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ninasema, Serikali imejipangaje kudhibiti wizi wa binadamu kwa jina maarufu ni utekeji, kwa kuwa Iringa tumeshapoteza vijana wetu wawili, Ndugu Banes Nyato na kijana mmoja anaitwa Ndugu Ally kwa kutekwa. Sasa Serikali imejipangaje kudhibiti wizi huo wa binadamu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu leta kama swali la msingi ili Serikali iweze kujibu kikamilifu.

Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Kalambo sasa aulize swali lake .

Na. 7

**Kuondoa Changamoto za Ushiriki wa Mambo ya Kijamii kati ya Tanzania na Zambia**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaondoa usumbufu wa kupata vibali na gharama pale raia wa Tanzania wanapolazimika kushiriki shughuli za kijamii Nchini Zambia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefunga mifumo ya kielektroniki katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili kurahisisha upatikanaji wa hati za safari (pasipoti) na hati za dharura za safari kwa lengo la kuwaondolea usumbufu raia wa Tanzania pale wanapohitaji hati

hizo kwa ajili ya kushiriki shughuli za kijamii katika nchi jirani. Kwa raia wanaoishi ndani ya eneo lisilozidi kilometa 10 kutoka mpaka wa nchi yetu na nchi jirani na wananchi wanapokuwa na shughuli za dharura kama vile misiba na magonjwa, hupatiwa ruhusa maalum kuwawezesha kwenda umbali usiozidi kilomita 10 ili waweze kushiriki shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa wale wanaoenda nchi jirani kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, wanapaswa kufuata sheria na taratibu za nchi husika katika kulipia vibali vinavyoendana na shughuli wanazoenda kufanya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba niulize maswali madogo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa mwananchi wa kawaida ambaye anaenda kushiriki shughuli za kijamii kutozwa kibali shilingi 20,000 ni gharama kubwa sana. Je, Serikali itakuwa tayari kupunguza tozo hizo ili walau iwe shilingi 5,000 au shilingi 2,000 ikiwezekana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ninashukuru Serikali wamefunga vifaa vya kielektroniki, ninataka kujua katika Wilaya ambazo zimenufaika na Wilaya ya Kalambo ni miongoni mwao? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tozo hizi za shilingi 20,000 zipo kwa mijibu wa sheria pale ambapo tutaona kuna haja ya kupunguza basi Serikali itayafanyia kazi mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, nadhani ameipongeza Serikali kuweka mifumo ya kielektroniki ambapo Wilaya ya Kalambo pia imenufaika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa uraia wa makazi ya Mishamo, Ulyankulu na Katumba. Utaratibu uliopo kwa sasa wanaingia na kutoka kwa vibali. Je, ni lini Serikali itatoa vizuizi na mageti yaliyopo kwenye makazi ya Mishamo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso swali lako kwa ninavyomwona Mheshimiwa Naibu Waziri hapa, ni kama swali limetoka nje kidogo na linahitaji kuwa amefanyia kazi hilo eneo mahususi, yaani siyo swali la jumla na ni la nyongeza, hilo la vibali lazima akafuatilie. Mheshimiwa Naibu Waziri utampatia Mheshimiwa Mbunge majibu mahsusi kwa hilo eneo analolisemea wananchi kuingia na kutoka kwa vibali.

Tunaendelea, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa, ninaona mmesimama wawili sasa nani mwenye majibu?

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, mimi ndiyo nimepata kibali kwa Maida.

**SPIKA:** Wewe ndiyo una majibu kwa Maida, haya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma kwa niaba ya Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah. *(Kicheko)*

Na. 8

**Malipo ya Madai ya Askari Polisi Waliomaliza Muda Wao**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA K.n.y. MHE. MAIDA HAMADI ABDALLAH** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa madai ya muda mrefu Askari Polisi waliomaliza muda wao?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kulipa madai ya askari Polisi waliomaliza muda wao wa kazi baada ya kustaafu, jumla ya fedha kiasi cha shilingi 97,120,011,700.26 zinadaiwa. Mpaka sasa madai yaliyohakikiwa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo ni shilingi 75,214,744,005.10. Kwa sasa madai yanayoendelea kuhakikiwa ni ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kiasi cha fedha shilingi 21,905,267,695.16 zinadaiwa.

Mheshimiwa Spika, pindi uhakiki ukikamilika madai yote yatawasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdulla Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mwanana ya swali hili. Tumekuwa tukihimiza sana matumizi ya *IT* (mfumo wa kidijiti) kwa watumishi wote.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, ni kwa nini ripoti zisiwekwe vizuri ili mfumo huu urekodi mambo yote ya mahitaji anayotakiwa kulipwa askari mstaafu (mafao yake na kila kitu chake); badala ya ile siku ya mwisho anapomaliza kazi kumtaka athibitishe alianza lini, alipandishwa cheo lini na alikopa kitu gani, jambo ambalo linaleta usumbufu?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inatambua kwamba askari hawa wanayahitaji zaidi mafao hayo kuliko siku nyingine yoyote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Juma kama iofuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Jeshi la Polisi lipo katika maboresho makubwa sana ya kuweka mfumo wa kielektroniki ili kuhakikisha kwamba taarifa zote za askari zinaingia kwenye

mfumo huo ili kuepuka usumbufu wakati wanapomaliza muda wao wa kazi na kupata madai yao kwa muda. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

Na. 9

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Polisi Msalala**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y. MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Makao Makuu ya Polisi katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ina kituo cha polisi daraja B ambacho kinakidhi mahitaji ya kutoa huduma ya polisi kwa wananchi wa Msalala. Kituo hiki kipo eneo la Bugarama na kina miundombinu yote ya msingi ikiwemo Ofisi za Mkuu wa Polisi wa Wilaya *(OCD),* Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Wilaya *(OC-CID),* Mkuu wa Kituo *(OCS),* Ofisi ya Makosa ya Usalama Barabarani pamoja na Ofisi ya Dawati la Kushughulikia Ukatili wa Kijinsia. Kituo hiki kitatumika kama Makao Makuu ya Polisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kahama. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Iddi Kassim, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza; Serikali iliahidi kujenga nyumba za watumishi wa Jeshi la Polisi pamoja na viongozi katika Wilaya ya Hai; je, ni lini Serikali itaanza kujenga nyumba hizi za watumishi?

Swali la pili; kwa kuwa wamesema pale Msalala ni makao makuu, je, hawaoni kuwa ipo haja ya kujenga nyumba za watumishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, ya Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna upungufu wa nyumba za watumishi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Hai na Wilaya ya Msalala kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, nyumba hizi tunazijenga kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi wetu ambao ni askari katika maeneo ya Hai pamoja na Msalala kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Mbarali, sasa aulize swali lake.

Na. 10

**Zoezi la Anwani za Makazi kwa Maeneo ambayo bado - Mbarali**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya zoezi la Anwani za Makazi katika baadhi ya maeneo ya Rujewa, Imalilo, Songwe na Mwatenga ambayo bado hayajafanyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi ulifanyika Februari hadi Mei 2022 kwa njia ya operesheni. Hatua hii ilikuwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoyatoa tarehe 8 Februari, 2022. Kupitia Operesheni ya Anwani za Makazi Mfumo wa Anwani za Makazi ulitekelezwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi ni endelevu kwa sababu ya mabadiliko ya makazi, wakazi na huduma. Ili kuweka mazingira endelevu ya utekelezaji kila mkoa na halmashauri ina mratibu/waratibu wa kusimamia utekelezaji, uendelezaji na matumizi ya mfumo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI itatuma wataalam wake katika Halmashauri ya Mbarali kufanya ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kutembelea maeneo yaliyoainishwa na Mheshimiwa Mbunge ili kubaini mapungufu kwa ajili ya kuchukua hatua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, na ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri. Ninaomba ufafanuzi kupitia maswali mawili.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; katika maelezo ya Serikali wamesema kwamba ilikuwa ni operesheni maalum kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais; lakini tunafahamu operesheni huwa inafanyika kwa kipindi maalum. Sasa twende na lipi, ni zoezi endelevu au ni operesheni?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kama ni zoezi endelevu, ni lini sasa maeneo yetu ya Mbarali ambayo yametoka hifadhini na kurudishwa kwa wananchi yatawekwa vibao vya anuani za makazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba arudie swali namba mbili.

**SPIKA:** Maeneo yale ambayo yamerejeshwa kwa wananchi kutoka kwenye hifadhi, lini yatawekewa alama za anuani za makazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo. Kwanza, napokea pongezi na yeye pia ninampongeza sana kwa sababu anafuatilia sana mambo mengi yanayohusiana na masuala ya mawasiliano na teknolojia ya habari katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, suala hili lilianza kama operesheni maalum, lakini baada ya kufikia kiwango ambacho kiliridhisha, Mheshimiwa Rais aliporidhika, sisi kama Wizara tumefanya hii kuwa ni kazi endelevu kama ambavyo yeye ameuliza swali lake namba mbili.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya makazi yanaendelea kutokea mara kwa mara, majina ya makazi na vilevile teknolojia inavyoendelea kubadilika na biashara za mtandao zinavyoendelea kukua tunaendelea kuhitaji sana suala hili la anuani za makazi.

Mheshimiwa Spika, kwa swali namba mbili, niseme kwamba, maeneo haya ambayo yamerejeshwa tutatuma wataalam kwenda kwa Mheshimiwa Mbunge ili kulifanyia kazi na kuhakikisha nao pia wanapatiwa huduma hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 11

**Ujenzi wa Mnara wa Simu Kerebe – Muleba**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga mnara wa simu katika Kata ya Kerebe Muleba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Tanzania ya Kidigitali wa Awamu ya Kwanza *(DTP)* ambapo mkataba wake ulisainiwa tarehe 13 Mei, 2023 na utekelezaji unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 12 Mei, 2025. Kupitia mradi huu Kata ya Kerebe imejumuishwa na kupata mtoa huduma wa Vodacom.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mnara huu wa *Vodacom* katika Kata ya Kerebe upo katika hatua za awali ambapo mtoa huduma ameanza uchimbaji wa msingi na ujenzi wa mnara huu. Aidha mnara huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Februari 2025. Hivyo, kukamilika kwa mradi huu kutaboresha huduma za mawasiliano ya simu katika kata hiyo, ambapo mnara huu umelenga kunufaisha Kijiji cha Makibwa na vijiji vingine vya jirani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, ni lini sasa Serikali itasimamia wanaojenga minara hii ya ziwani waweze kuweka taa kwa ajili ya kuwamulikia wale wavuvi wote wanaosafiri wakati wa usiku ziwani katika visiwa vyote vya Wilaya ya Muleba?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, ni lini Serikali itajenga mnara katika Kijiji cha Nterungwe Kamata ya Nyamiaga katika Jimbo la Ngara ambapo hakuna mawasiliano kabisa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kuweka taa kwenye minara ninapenda kusema kwamba nimelipokea. Tayari kuna baadhi ya maeneo tulipewa maombi hayo na tukafanya, basi naahidi na eneo hili pia tutalizingatia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa suala la kata hii aliyoitaja, kuhusiana na ujenzi wa mnara katika eneo hili la Ngara tutaendelea pia kuweka makadirio ya kuhakikisha maeneo yote ambayo minara bado haijajengwa, inajengwa na kuboresha hali ya mawasiliano maeneo yote nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, sasa aulize swali lake.

No. 12

**Mradi wa Maji ya Ziwa Tanganyika**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Tanganyika ili kumaliza changamoto ya maji Nkasi umefikia wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mkakati wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kwa ajili ya kutatua changamoto ya maji katika Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa ikiwemo Wilaya ya Nkasi. Serikali kwa sasa ipo katika hatua za mwisho za kumpata mtaalam mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina wa mradi huo ambapo unatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ninatambua jitihada za Serikali kwenye jambo hili muhimu, lakini majibu ya Serikali wanasema mwezi Aprili mwaka huu ndio wanategemea angalau hatua za usanifu wa kina zitaanza. Swali la kwanza; je, wana mpango mkakati gani kwa kipindi hiki wa kuleta mradi wa muda mfupi wakati tunasubiri mradi huo wa muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pamoja na kwamba ni mradi ambao utatumia gharama kubwa, Mamlaka ya Mji Mdogo Namanyere upatikanaji wa maji ni 49% huku upotevu wa maji ni ukiwa ni 43%; ni asilimia sita tu ndiyo inayowafikia wananchi, na tunahitaji shilingi bilioni 1.8; je, ni lini wataleta fedha hizo kabla ya kuleta Mradi huo mrefu wa Kutoa Maji Ziwa Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninatambua na Serikali pia inatambua changamoto ya maji na imekuwa na mkakati wa muda mfupi, wa kati na mrefu. Tunatambua Mheshimiwa Aida anawasilisha changamoto ya wananchi wake; lakini Serikali ina mkakati na programu ya visima 900 ambapo tunaendelea navyo. Kwa upande Mheshimiwa Aida tuna upande wa Ninde, Kipili pamoja na *Isale Group* kuna mradi huo wa vijiji sita, pamoja na Paramawe.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa kwamba huu ni mkakati ambao utasaidia kutatua changamoto kwa kipindi ambacho tunaendelea na utekelezaji wa mradi wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inatambua upotevu wa maji katika mji mdogo; na hii ni kwa sababu ya miundombinu kuwa chakavu. Sasa Serikali tulitenga kiasi cha shilingi milioni 815 ambazo zitashughulikia miundombinu na kurekebisha maeneo ambayo miundombinu yake imechakaa ili kuhakikisha kwamba tunaondoa upotevu wa maji kutoka 43% kwenda katika 25% inayokubalika kimataifa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatoa maji Ziwa Victoria kupitia Mradi wa Mugango – Kiabakari – Butiama kuja Nyamuswa na kusamba Jimbo Zima la Bunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi kutoka Mugango – Kiabakari tayari umekwishakamilika 100% na wananchi wanapata huduma ya maji kutoka Butiama. Kuhusiana na kupeleka upande wa Nyamuswa tumesanifu mradi wa shilingi bilioni nane na tayari mkandarasi ameshapatikana. Tunatarajia ifikapo mwezi Februari mkandarasi ataanza kazi mara moja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Rashidi Abdallah Shangazi.

Na. 13

**Uwiano wa Daktari na Mgonjwa Nchini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, upi uwiano wa madaktari na wagonjwa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa niaba ya Wizara ya Afya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI k.n.y. WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hapa nchini uwiano wa madaktari na wagonjwa ni madaktari 8.4 kwa kila watu 10,000. Uwiano huu ni sawa na theluthi moja ya viwango vilivyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani kwa nchi zinazoendelea ambapo inapendekezwa uwepo wa uwiano wa Madaktari 22.8 kwa kila watu 10,000. Aidha kwa nchi zilizoendelea uwiano ni Madaktari 2.4 kwa watu 1000.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba majibu ya Mheshimiwa Waziri ni sahihi na Wizara hii siyo ya kwake lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa madaktari wengi wako katika ngazi ya *degree* (shahada ya kwanza) lakini huku chini kwenye vituo vya afya pamoja na zahanati kuna *Assistant Medical Officers* na *Clinical Officers* ndio wanaohudumia jamii kubwa ya Watanzania. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba katika hizi ngazi za msingi tunakuwa na *Assistant Medical Officers* na *Clinical Officers* wengi zaidi kuliko hao madaktari wa ngazi ya *degree*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI K.n.y. WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Shangazi kwa niaba ya muuliza swali Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudi za kutoa vibali kwa ajili ya kuajiri madaktari ambao wame-*qualify (Degree holders wa Medical Doctors)* kwa mwaka juzi iliajiri madaktari 1,200 na mwaka jana 2023/2024 imeweza kuajiri madaktari 1,500. Wakati huo huo Serikali inaendelea kutoa vibali kwa ajili ya kuajiri *paramedical* pamoja na wale madaktari wa chini *(Assistant Medical Officers, Clinical Officers* na *Assistant Clinical Officers)* kwa ajili ya ku-*support* hii kada ya udaktari kwa kutoa huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, ni kwamba Serikali imeendelea kutoa vibali na watumishi wa afya kwa ujumla wanaendelea kuajiriwa; na mwaka huu Serikali imeajiri watumishi zaidi ya 12,000.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Serikali Kuingia Ubia na Hospitali ya *ALMC***

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je Serikali ina mpango gani wa kuingia ubia na Hospitali ya *ALMC* Arusha ili kuiokoa na changamoto za kifedha zinazoikabili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI K.n.y. WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mchango wa Serikali katika Hospitali ya *Arusha Lutheran Medical Centre* unatolewa katika huduma za chanjo, huduma za VVU (miradi msonge), kifua kikuu pamoja na fedha za bidhaa za afya ambapo kwa mwaka kiasi cha shilingi milioni 536.8 kimetolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaanza kufanyia kazi ombi la Hospitali ya *Arusha Lutheran Medical Centre* kwa lengo la kuhakikisha inakamilisha mkataba wa makubaliano ya ubia kati ya Serikali na hospitali hiyo ili kuiwezesha kutoa huduma bora na endelevu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inachangia kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya malipo ya mishahara, fedha za dawa na vifaa tiba pamoja fedha za matumizi mengineyo katika Hospitali ya Seriani ambayo pia inamilikiwa na Kanisa la KKKT – Arusha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, swali langu la msingi ni kuhusiana na Hospitali ya *ALMC* na linahusiana na kuingia ubia. Swali la kwanza; je, Serikali inaweza ikatupa *time frame,* kwamba ni baada ya mwezi mmoja, miezi mitatu au miezi sita, hasa ukizingatia kwamba tunakwenda kwenye Mashindano ya *AFCON* na pia kuna *Royal Tour* pale Arusha na huduma za afya ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni kuhusiana na Serikali kusema kwamba imepeleka shilingi milioni 536.8. Hata hivyo kwa taarifa nilizonazo Serikali imepeleka shilingi milioni 130 kwa ajili ya ruzuku za dawa. Je, tunaweza tukapata mchanganuo wa shilingi milioni 406.8 ambazo zimesemwa hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa amekuwa mstari wa mbele sana katika kuhakikisha kwamba anaipambania hospitali hii ili ipate fedha na iingie ubia na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa ya kufuatailia matumizi ya hospitali hii (matumizi na fedha wanazokusanya) ambapo tumekuja kugundua kwamba kuna baadhi ya changamoto katika hospitali hiyo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge tukitoka hapa nimweleze kuhusiana na changamoto zilizomo mule ndani ili aende akatoe ushauri. Serikali baada ya kuona imetatua changamoto hizo za ndani za hospitali hiyo, ninadhani Serikali itakuwa tayari katika kuendelea kutoa msaada zaidi kuhakikisha hospitali hiyo inaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kutambua kwamba hospitali hizi ambazo zinamilikiwa na mashirika binafsi zimekuwa zikitoa msaada kwa Serikali na Serikali imekuwa ikitoa fedha ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma kupitia hospitali hizo kwa sababu wote tunaenda kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la *time frame* ninaomba niendelee kusema kwamba *time frame* siwezi kutoa mpaka pale changamoto zitakapokuwa zimetatuliwa, hapo sasa inawezekana tukaenda kufikia muafaka.

Mheshimiwa Spika, mwisho, swali la pili ameuliza kuhusiana na mchanganuo wa fedha zilizotolewa. Serikali inatoa fedha kwa awamu. Fedha hizi ambazo tumesema tunakwenda kuzitoa mwaka huu zipo ndani ya bajeti na fedha ambayo imekwenda ni ile ambayo inakwenda hatua kwa hatua. Kwa hiyo, fedha inavyoendelea kupatikana tunaendelea kutoa fedha katika hospitali hiyo kwa ajili ya uendeshaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 15

**Halmashauri ya Wilaya ya Maswa Kupewa *CSR***

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza: -

Je, lini Halmashauri ya Wilaya ya Maswa itapewa *CSR* inayotokana na uwepo wa Mradi wa *SGR*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mikataba ya ujenzi inayoingiwa kati ya *TRC* na mkandarasi imeendelea kuzingatia suala la uwajibikaji kwa jamii yaani *Corporate Social Responsibility (CSR)* kwa kutenga fedha. Aidha, Mradi wa Ujenzi wa Reli ya *SGR* umeendelea kutoa *CSR* katika maeneo ambapo mradi unapita na mpaka sasa mradi umefadhili miradi mbalimbali yenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 9.5. Kwa upande wa Wilaya ya Maswa, kwa kuanzia Mradi wa Ujenzi wa Reli ya *SGR* kwa kipande cha Isaka-Mwanza umeshatoa *CSR* yenye thamani ya shilingi milioni 28.4 ambazo kwa kuanzia zimeelekezwa kwenye mradi wa bweni la wanafunzi katika shule ya Sekondari ya Wasichana Mataba, Mwasalage na ujenzi wa Shule ya Sekondari Mashimba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali na sina swali la nyongeza. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan.

Na. 16

**Vyombo vya Usafiri Majini Kuwa na Vifaa vya Uokozi**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN K.n.y. MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza:-

Je, ni kiasi gani Serikali inahakikisha vyombo vya usafiri majini vinatimiza takwa la kuwa na vifaa vya uokozi kwa abiria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TASAC* inachukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha vyombo vya usafiri majini vinatimiza takwa la kuwa na vifaa vya uokozi kwa abiria. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ukaguzi wa vyombo vyote vya usafiri majini na utoaji wa vyeti vya ubora. Ukaguzi huu unahakikisha vyombo vina vifaa vya uokozi kama maboya ya kujiokoa kwa abiria wote;

(ii) Kutoa elimu kwa jamii na kampeni maalum kwa jamii zinazoishi maeneo yanayozungukwa na maji. Lengo ni

kuwafundisha wamiliki wa vyombo na abiria umuhimu wa vifaa vya uokozi na taratibu za usalama; na

(iii) Kampeni za usalama wakati wa sikukuu ili kuhakikisha havizidishi idadi ya abiria iliyoainishwa kwenye vyeti vyao. Vyombo vinavyoshindwa kufuata sheria hupigwa faini hadi shilingi milioni 6.25 kwa vyombo vikubwa (zaidi ya mita 24) na shilingi laki nne kwa vyombo vidogo (chini ya mita 24).

Mheshimiwa Spika, vilevile Tanzania kupitia *TASAC* inatekeleza mikataba ya Shirika la Bahari Duniani yaani *International Maritime Organization (IMO)* kama *SOLAS (Safety of Life at Sea Convention)*. Mkataba huo wa lazima kwa nchi mwanachama pamoja na mambo mengine unalazimisha vyombo vya usafiri majini kuwa na vifaa vya uokozi ambavyo vinakidhi viwango vya kimataifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Bakar hana swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, nimeletewa hapa ujumbe na watu watatu kwa wakati mmoja kwa hivyo yule ambaye amepewa majibu ya msingi ya haya maswali ndiye ambaye aendelee kusimama. Hapa nina jina la Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, Mheshimiwa Shally Raymond na wote bado mmesimama. Pia, yupo Mheshimiwa Stella Ikupa Alex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, nina majibu ya msingi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba uketi mwenye majibu yupo tayari kwa ajili ya kuuliza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nipo tayari kumwachia Mheshimiwa Ikupa lakini ni kweli alinipigia saa 12 asubuhi.

**SPIKA:** Sijakuelewa, umesema?

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, pia aliniomba nimuulizie hilo swali saa 12 asubuhi ya leo, lakini ninamwachia Mheshimiwa Ikupa kama ana majibu.

**SPIKA:** Sawa na wa nyuma yako pia alipigiwa simu kwa hiyo ndiyo maana nimeuliza. Mheshimiwa Shally Raymond pia amepigiwa simu ndiyo maana nimeuliza mwenye majibu kati yenu ni nani na mwenye majibu ni Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, sasa aulize swali kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 17

**Pori la Pande - Dar es Salaam Kuwa Kivutio cha Utalii**

**MHE. STELLA I. ALEX K.n.y MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza Pori la Pande lililopo Dar es salaam kuwa kivutio cha Utalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, pori la akiba la Pande ni pori pekee lililopo katika Jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya misitu ya Ukanda wa Pwani. Kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ilijenga miundombinu mikubwa ya maeneo ya kupumzikia wageni na kambi za watalii katika eneo hilo. Vilevile, mwaka 2023/2024 Wizara imeanzisha bustani ya wanyamapori na kuweka wanyama katika eneo hilo ambapo mpaka sasa, pori hilo lina idadi ya wanyama zaidi ya 100. Aina za wanyama waliopo sasa ni duma, mamba, simba, pundamilia, nyumbu, swala granti, swala pala na nyoka wa aina mbalimbali akiwemo chatu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, miundombinu ya barabara katika pori hilo imeboreshwa na inapitika katika kipindi chote cha mwaka na Wizara imejenga lango kuu la kuingilia kwenye pori hilo. Kufuatia juhudi hizo, idadi ya watalii wanaotembelea pori hilo imeendelea kuongezeka ambapo kuanzia mwaka 2023 hadi 2024 watalii 4,606 wameweza kutembelea. Aidha, Wizara imetenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji katika miundombinu ya michezo ya watoto yenye kiwango cha kimataifa pamoja na huduma za malazi. Hivyo, wawekezaji wanakaribishwa kutumia fursa hii kuwekeza kwenye pori hilo kwa lengo la kukuza utalii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanyika katika pori hili. Swali la kwanza; ni nini mkakati wa Serikali kuongeza wanyama katika pori hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pia, kwenye jibu la msingi imeeleza tu kwamba uwekezaji uliopo sasa hivi ni kwenye miundombinu ya michezo. Tunaomba kufahamu kama kuna uwekezaji mwingine ambao unapatikana katika pori hili? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba idadi inaonekana ni ndogo, lakini tuna mpango wa kuongeza wanyama kwenye eneo hili. Tutakuwa tunaongeza taratibu kulingana na ikolojia ilipo na uwezo wa kuhimili wanyama hao kupokelewa. Pia, kwenye eneo la uwekezaji tumesema kwamba ukiacha kuwekeza kwenye viwanja vilevile tunatoa fursa kwenye kuwekeza maeneo ya malazi ndani ya eneo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 18

**Kuwalipa Wateja wa *Kagera Cooperative Bank***

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa wateja walioweka fedha zao katika *Kagera Cooperative Bank*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Januari 4, 2018, Benki Kuu ya Tanzania iliifutia leseni ya biashara benki ya wakulima Mkoa wa Kagera na kuiteua Bodi ya Bima ya Amana kuwa mfilisi wa benki hiyo. Hadi Desemba 2024, jumla ya shilingi milioni 846.16 kati ya shilingi milioni 899.56 sawa na 94.06% zilimelipwa kama fidia ya bima ya amana kwa wateja 1,391 waliojitokeza kati ya wateja 2,797 waliokuwa na amana isiyozidi shilingi 1,500,000. Aidha, katika kipindi hicho, Bodi ya Amana imelipa wadai wa benki fidia ya ufilisi shilingi milioni 664.25 kati ya madai ya shilingi bilioni 1.64 sawa na 40.50% kwa wateja 195 kati ya wateja 274 wanaostahiki kulipwa fidia hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kuhamasisha wananchi wanaodai fedha zao kuwasiliana na Bodi ya Bima ya Amana ili kulipwa stahiki zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ni miaka nane sasa tangu Benki ya

Wakulima ya Kagera kufungwa, lakini waliokuwa na amana au fedha zaidi ya shilingi milioni moja na nusu wamelipwa 43% tu ya fedha walizokuwa wameweka benki, ni lini Serikali itawalipa watu hawa 57% ya fedha zao zilizobaki benki kwa sababu wanateseka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa watumishi waliokuwa kwenye benki hiyo walilipwa nauli tu wakaahidiwa kulipwa stahiki zao, ni lini stahiki zao za kiutumishi zitalipwa kwa sababu hawajalipwa hata senti tano mpaka leo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu ninaomba kumpongeza sana kwa namna anavyofuatilia kwa karibu sana suala hili. Hii 40% ambayo tumefika kuna mchango wake mkubwa sana pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Spika, malipo yanaendelea kulipwa na dirisha bado halijafungwa. Kwa hiyo tuendelee kuhamasisha watu wetu wadai, wawasiliane na Bodi ya Bima ya Amana ili kulipwa madai yao. Kuhusu watumishi, haya ni masuala ya kiutumishi. Ninaomba hili tulichukue nikae naye na watu wetu wa utumishi ili tuweze kuwasaidia watumishi wetu hawa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, wananchi Jimbo la Mtwara Mjini wanadai taasisi ya *PRIDE* ambayo ilikuwa inatoa mikopo kwa wananchi takriban shilingi milioni 500. Kwa sasa, zaidi ya miaka 15 watu hao wanahangaika na hawajapata malipo yao. Je, ni lini Serikali mtakwenda kuwapatia fedha zao wale wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, una uchaguzi wa kujibu hilo swali au lije kama swali la msingi kwa sababu liko mahususi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba lije kama swali la msingi.

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Mbunge, litakuja kama swali la msingi ili uweze kupata majibu mahususi kwa jambo ambalo umeliuliza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Kukamilisha Maboresho ya Kanuni za Uvuvi**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha maboresho ya Kanuni za Uvuvi ili kupata ufumbuzi wa aina ya wavu wa kuvulia samaki aina ya migebuka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikifanya maboresho katika Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009. Aidha, Kanuni hizi zimekuwa zikiboreshwa kila mara ambapo mwaka 2018, 2019, 2020 na 2022 maboresho yalifanyika ili kukidhi mahitaji ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za uvuvi nchini. Hata hivyo, Wizara imekamilisha utaratibu wa kutoa Waraka wa Matumizi ya Wavu wa Makila kwa ajili ya uvuvi wa samaki aina ya migebuka katika Ziwa Tanganyika ambapo, Waraka huu utakuwa ni hatua

za haraka na za awali katika kutatua changamoto inayowakabili wavuvi katika Ziwa Tanganyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mwaka 2022 maboresho yaliyofanyika katika Kanuni hizi za Uvuvi hayakugusa wavu huo unaovua samaki aina ya mgebuka na huyu ndiye samaki ambaye anapatikana kwa wingi katika Ziwa Tanganyika. Kwa muda wa miaka mitano tangu nimekaa katika Bunge hili tunazungumza Kanuni hii tu bila kufikia mwisho. Ni lini tutafikia mwisho wa suala la kupata kanuni inayoruhusu wavu wa kuvua samaki wa mgebuka na kanuni nyingine zinazohusu usalama katika Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, kwa sasa Waraka unakamilishwa na upo hatua za mwisho kwa ajili ya kuja kutatua tatizo hili ambalo linahusu wavuvi ambao wanahusika sana katika uvuvi wa samaki aina ya migebuka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, awe na matumaini jambo hili linaenda kutatuliwa hivi karibuni. Miaka mitano tuisahau sasa tuko kwenye kipindi cha utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA**: Mheshimiwa Spika, je, Serikali ipo tayari kuboresha kanuni za uvuvi ili 10% ya mapato ya Sekta ya Uvuvi yanayopaswa kurejeshwa kuendeleza sekta iweze kutekelezeka kama sheria inavyotaka ili wanawake wanaojihusisha na sekta hii waweze kuepuka changamoto wanazopitia kwa kutumia miundombinu isiyo rafiki wakati wa kwenda kununua samaki kama vile kujenga maeneo ya kununulia samaki kwenye mialo yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, tunaendelea na matayarisho ya waraka na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge muda mfupi ujao haya ambayo unayaeleza yanaenda kuwa katika muundo wa kimaandishi ili wananchi waweze kunufaika na utekelezaji wa zoezi la uvuvi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 20

**Ujenzi wa Majosho Halmashauri ya Itigi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, majosho mangapi yatajengwa katika Halmashauri ya Itigi katika Mwaka huu wa Fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilijenga majosho saba yenye thamani ya shilingi 161,000,000 katika Kata ya Kitaraka yalijengwa majosho mawili, Mwamagembe josho moja, Idodyandole josho moja, Mitundu josho moja, Mtakuja josho moja na Majengo josho moja, katika Halmashauri ya Itigi. Aidha, Wizara itaendelea kuweka katika mpango wa bajeti ya mwaka 2025/2026, ujenzi wa majosho nchini yakiwemo majosho katika Halmashauri ya Itigi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE**: Mheshimiwa Spika, ninaomba unipe dakika moja nikushukuru wewe, ofisi yako, Ofisi ya Katibu wa Bunge. Pia ninashukuru sana Kituo cha Afya Bunge, Hospitali ya Rufaa ya Benjamin Mkapa, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Shirika la Bima *(NHIF)* kwa huduma ambayo mmenipatia wakati nikiwa katika hali ngumu. Ninawashukuru sana wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninasimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa na afya njema kuwakilisha wananchi wangu wa Jimbo la Manyoni Magharibi. Ninashukuru sana na sina swali la nyongeza, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Serikali, ninaomba nijue kuhusu majosho Mbogwe; mwaka jana yalikuwepo kwenye bajeti na hata mwaka huu yapo. Ni lini sasa utekelezaji wake utafanywa ili majosho hayo ya Mbogwe yakamilike? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Maganga. Mbogwe itakuwa miongoni mwa majosho yanayowekwa kwenye mpango wa bajeti ya 2025/2026. Mheshimiwa Mbunge, tuwe na subira kidogo tu, tutapata mahitaji haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Jimbo la Igunga ni moja ya majimbo yenye mifugo mingi sana nchini. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga majosho kwenye Kata za Mwamashiga, Mwamashimba na Mwamakona? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu katika swali la msingi ni kwamba tumeweka katika Mpango wa Bajeti inayokuja ya mwaka 2025/2026 kuendeleza ujenzi wa majosho yote hapa nchini yakiwepo majosho ya Mheshimiwa Ngassa kule Igunga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ni lini Serikali itaanza ujenzi wa majosho manne ambayo yamekuwa yakitokea kila mwaka wa bajeti ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojieleza kwenye jibu langu la msingi, tunaliweka kwenye makadirio ya fedha ya kipindi cha 2025/2026 ambapo tunakwenda kujenga majosho mengi kwa nchi nzima na jimbo la Chemba litakuwa sehemu ya mradi huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta tangazo nililonalo hapa mbele, ni tangazo la wageni.

Kwanza, tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Yupo mgeni mmoja wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani ambaye ni mwanafunzi kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Mgeni mmoja wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ndugu yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, wapigakura wake kutoka Jimbo la Bunda, Mkoani Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 29 wa Mheshimiwa Mary Masanja ambao ni Wauguzi kutoka Mkoa wa Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni mmoja wa Mheshimiwa Esther Malleko ambaye ni Mwinjilisti kutoka Usharika wa Chinangali, Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Janejelly Ntate ambao ni Wanakwaya wa Chuo cha Mipango Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi watano na wafanyakazi sita kutoka Shule ya Msingi ya Kiingereza ya Bohari iliyopo Wilaya ya Karagwe, Mkoani Kagera. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 24 na walimu tisa wa Shule ya Sekondari Mwanza iliyopo Wilaya ya Nyamagana, Mkoa wa Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 45 wa Taasisi ya Taaluma za Maendeleo ya Jamii (*IDS*) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni, ninaona bendi yetu imeamua ikae na sisi mpaka sasa nayo basi niwatambulishe. Kipekee kabisa tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya ya kutuanzishia Bunge letu, ahsanteni sana na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.41 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 29 Januari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*